[Namba: 2]

# سُؤَالٌ وَجَوَابٌ

# فِيْ

# أَحْكَامِ الصِّيَامِ

# SWALI NA JAWABU

# KUHUSU

# HUKUMU ZA SAUMU


**Mtunzi:**

**Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Uthaymin**

**Tarjama:**

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

بسم الله الرحمن الرحيم

# MAMBO AMBAYO HAYAVUNJI SAUMU/FUNGA

1. **Kupiga mswaki kwa kutumia dawa ya meno, kupaka wanja, kuweka dawa ya matone katika macho au masikio.**

**Swali:** Ni ipi hukumu ya kupiga mswaki baada ya kupinduka jua (kuanzia wakati wa adhuhuri) kwa mtu aliyefunga?

**Jawabu:** Ni sunna kwa mtu aliyefunga kupiga mswaki, kabla ya kupinduka jua au baada yake, kama ilivyokuwa sunna kwa mtu ambaye hajafunga (wote sawa), kwa sababu hadithi zilizokuja kuelezea sunna ya kupiga mswaki ni zenye kuenea kila wakati, wala hazijamvua katika sunna hiyo mtu aliyefunga, wala kumuwekea wakati wa kabla ya kupinduka jua au baada yake.

**Swali:** Ni ipi hukumu ya kupiga mswaki kwa kutumia dawa ya meno wakati wa mchana kwa mtu aliyefunga?

**Jawabu?** Kupiga mswaki kwa kutumia dawa ya meno wakati wa mchana kwa mtu aliyefunga, ni sawa iwe katika mwezi wa Ramadhani au miezi mingine, hakuna tatizo endapo haikupita kwenye koo na kuingia tumboni, lakini iliyo bora ni kuacha kutumia, kwa sababu inapenya kwa haraka (kuingia tumboni), kwa hiyo huenda ikapita na kuingia tumboni hali ya kuwa mtu hajui.

**Swali:** Ni ipi hukumu ya kupaka wanja, au kuweka dawa ya maji (matone) ya jicho au sikio kwa mtu aliyefunga?

**Jawabu:** Hapana vibaya kwa mtu aliyefunga kupaka wanja, kuweka dawa machoni au sikioni, hata kama atahisi ladha (ya dawa) katika koo yake bado hajafungua, lakini kama ataweka dawa hiyo puani na ikashuka mpaka tumboni basi amefungua, endapo alikusudia kufanya hivyo.

**Swali:** Je, mtu kuvuta/kunusa harufu nzuri, kama vile manukato, udi n.k., kunaharibu saumu/funga yake?

**Jawabu:** Aina zote za mafuta mazuri/manukato ambayo hayana kitu chenye kuingia puani (ni hewa tu), basi hayavunji saumu ya mtu, lakini ikiwa harufu/manukato hayo yana moshi (kama vile udi au ubani), kisha mtu akaumeza moshi huo mpaka ukaingia tumboni mwake basi amefungua, na ikiw ni kujifukiza tu bila kumeza hapana tatizo.

2. **Hukumu ya kumeza mate, udenda, kohozi na kamasi kwa mtu aliyefunga:**

**Swali:** Je, kumeza mate kunaharibu saumu/funga ya mtu?

**Jawabu:** Kumeza mate hakuharibu saumu ya mtu.

**Swali:** Ni ipi hukumu ya mtu kumeza udenda au kohozi/kamasi kwa mtu aliyefunga?

**Jawabu:** Ikiwa atameza (udenda, kohozi au kamasi) hali ya kuwa bado vipo mdomoni mwake, basi funga yake ni sahihi, lakini kama alilitoa (kohozi n.k) mpaka nje ya midomo yake kisha akalivuta tena mdomoni na kulimeza, basi atakuwa amefungua na funga yake imaharibika. Na wapo katika maulamaa waona kwamba bado hajafungua, na hii ndio kauli aliyoichagua sheikh Ibn Uthaymin (Allaah amrehemu).

3. **Kuonja chakula, kuogolea, kusukutuwa na kuyavuta maji puani:**

**Swali:** Je, kuonja chakula kunaharibu funga ya mtu

**Jawabu:** kuonja chakula hakuharibu funga ya mtu, endapo hatomeza, lakini mtu asifanye hivyo mpaka awe anahitajia.

**Swali:** Ni ipi hukumu ya kuogolea kwa mtu aliyefunga?:

**Jawabu:** Hapana vibaya kwake kuogolea, na kuzama ndani ya maji kwa namna anavyotaka, lakini ajichunge kunywa maji na kuingia tumboni mwake, na pia kuogelea kunamtia nguvu mfungaji…

**Swali:** Je, ikiwa mfungaji amesukutuwa maji kinywani au ameyavuta maji puani, kisha yakapitiliza mpaka tumboni, atakuwa amefungua?

**Jawabu:** Ikiwa mfungaji atasukutuwa maji kinywani au kuyavuta maji puani, kisha yakapitiliza na kuingia tumboni atakuwa hajafungua, kwa sababu hakukusudia, na Allaah Ta'alaa anasema: **"Wala hapana lawama juu yenu kwa yake mliyokosea. Lakini ipo lawama kwa yale ambayo nyoyo zenu imeyafanya kwa makusudi".** **[Al-Ahzaab/5].**

### 4. Hukumu ya mtu kumkumbatia mkewe, au kuota (anafanya tendo la ndoa) mchana wa Ramadhani:

**Swali:** Je, inajuzu kwa mwenye kufunga kumkumbatia mkewe, (kumbusu) au kucheza mwili wake?

**Jawabu:** Ndio, inajuzu kwake kumkumbatia mkewe na kumchezea, isipokuwa akiogopea nafsi yake kwamba huenda akatokwa na manii, kwa sababu ikiwa atatokwa na manii kwa ajili ya kuyafanya hayo, basi funga yake itakuwa imeharibika/imebatilika, na itamlazimu kujizuia (bila kula) mchana mzima wa siku hiyo (hata kama funga yake imebatilika) na itamlazimu kulipa siku hiyo. Na kama itakuwa amefanya hayo katika saumu isiyokuwa Ramadhani, basi pia saumu yake itakuwa imebatilika, lakini si lazima kwake kujizuia na kula mchana mzima, labda ikiwa ni saumu ya wajibu (kama vile nadhiri, kafara, au akawa analipa masiku yaliyompita katika mwezi wa Ramadhani),

itamlazimu kuilipa siku hiyo. Lakini kama itakuwa ni saumu/funga ya sunna basi si wajibu kwake kuilipa.

**Swali:** Ikiwa mwenye kufunga ameota katika mchana wa Ramadhani, je, saumu/funga yake itabatilika?

**Jawabu:** Ikiwa mwenye kufunga ameota katika mchana wa Ramadhani, basi funga yake ni sahihi wala haijabatilika, kwa sababu hakufanya kwa hiyari yake, na pia mtu aliyelala kalamu haimuandikii yeye chochote (katika wema au ubaya).

5. **Kusengenya na kupeleka maneno ya umbea, na uchonganishi:**

**Swali:** Je, kusengenya na maneno ya umbea vinabatilisha saumu/funga?

**Jawabu:** Kusengenya na maneno ya umbea havibatilishi saumu/funga, lakini vinapunguza ujira wa saumu hiyo.

Wabillaahi Ttaufiq

**Namuomba Allaah aniruzuku Ikhlaas katika maneno na matendo**

**Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah**

**Pongwe Tanga**

**10/sha'ban/1444H – 3/3/2023H**

**Simu: 0715263253**